

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA DAR ES SALAAM**

Anwani ya Simu:

Simu: 2203156/2203158

Fax: +25522203213

Tovuti: [www.dsm.go.tz](http://www.dsm.go.tz)

Barua pepe : [ras@dsm.go.tz](mailto:ras@dsm.go.tz)



**OFISI YA MKUU WA MKOA,  
3, Barabara ya Rashid Kawawa,  
S.L.P. 5429,  
12880, DAR ES SALAAM.  
Tanzania**

**10 Agosti, 2020**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**RC KUNENGE AFANYA ZIARA YA KUTATUA KERO ZA WANANCHI PUGU**

Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Abubakar Kunenge leo tarehe 10 Agosti, 2020 amefanya ziara ya kusikiliza na kutatua kero za wananchi wa Pugu Stesheni ambapo ameahidi kuzipatia ufumbuzi kero mbalimbali zinazowakabili wananchi hao.

Katika ziara hiyo RC Kunenge amepokea changamoto mbalimbali zikiwemo za Elimu, Miundombinu, Maji, Umeme, Afya, migogoro mbalimbali ya Ardhi na changamoto za Kisheria ambapo zipo alizotatua papo kwa papo na nyingine kuzipatia utatuzi kwa kuwataka watendaji kuhakikisha wanazishughulikia Mara moja.

Kwenye ziara hiyo RC Kunenge aliambatana na watendaji mbalimbali wa Mkoa akiwemo Katibu Tawala wa Mkoa, Wakuu wa idara pamoja na Viongozi wa Wilaya ya Ilala.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano  
**OFISI YA MKUU WA MKOA  
DAR ES SALAAM**